



EAST AFRICAN
**CRUDE OIL
PIPELINE**

TANGAZO LA ZABUNI YA KUTOA HUDUMA ZA KIHANDISI ZA MATENGENEZO NA UKAGUZI - NAMBA YA KUMBUKUMBU: 10004944

Total east Africa Midstream B.V (TEAM) inawakaribisha makandarasi wenye uzoefu na sifa ambao wameonyesha uwezo, nia na ambao wako tayari kutoa huduma za kihandisi za matengenezo na ukaguzi kwenye miundombinu yote ya EACOP. Mradi wa EACOP unajumuisha bomba la mafuta lililofukiwa chini ya ardhi nchini Tanzania na Uganda likiwa na mfumo wa umeme wa kuleta joto pamoja na miundombinu iliyo juu ya ardhi na kituo cha kuhifadhia mafuta cha baharini na miundombinu ya kusafirishia mafuta nje ya nchi karibu na Tanga. Maendeleo ya mradi yanajumuisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na ukarabati wa bomba la mafuta ghafi kati ya Uganda na Tanzania na kituo kilicho baharini mjini Tanga, Tanzania. Uendelezaji unahusu pia ujenzi wa mabomba yanayoungwa kwenye bomba kubwa na kituo cha uchakataji nchini Uganda.

Maelezo mafupi kuhusu huduma

Mahitaji ya EACOP kwa ajili ya maandalizi ya mifumo ya matengenezo na ukaguzi wa miundombinu yanajumuisha ufanisi kwenye

usimamizi na upangaji, utekelezaji wa mfumo wa usimamizi wa matengenezo wa kikompyuta, maandalizi ya taratibu za matengenezo, tafiti kuhusu ukaguzi, utambuzi na manunuzi ya vipuri ikiwa ni pamoja na shughuli za manunuzi kabla ya kuanza uzalishaji ili kuwezesha shughuli zenye ufanisi.

Sifa za msingi:

- Uzoefu kwenye shughuli za matengenezo na ukaguzi wa miundombinu ya viwanda
- Uwezo wa kuandaa mfumo wa matengenezo ya miundombinu ya viwanda
- Taarifa zilizothibitishwa za utekelezaji wa shughuli za uhandisi za ukaguzi wa msingi wa hatari
- Weledi kwenye shughuli zinazohusiana na utambuzi wa vipuri
- Uanzishaji wa taratibu za usambazaji
- Stadi za kuunganisha, uwekaji vipaumbele na mipango
- Sera ya afya, usalama, mazingira, jamii na ubora
- Dhamira ya kutumia bidhaa za ndani

Makampuni yanayotaka kutuma maombi inabidi yawe na sifa za msingi na yawe na uwezo wa kutoa huduma zilizotajwa hapo juu, yaombe fomu ya zabuni kwa kutuma barua pepe kwa: ep.eacop.maintinsp.prequal@total.com kabla ya tarehe **2 Februari 2018, saa 11.00 jioni kwa saa za Kampala.**

Utoaji wa fomu ya maombi ya zabuni kwa makampuni husika utaendana na kusainiwa kwa Makubaliano ya Kutunza Siri (NDA), fomu itatolewa baada ya kampuni kupokea uthibitisho wa nia ya kushiriki. NDA itaonyesha tarehe ya kutolewa kwa majibu ya maombi.

Zingatia : Wazabuni waliopita kwenye mchujo tu ndio watakaalikwa kutuma maombi ya zabuni kwa ajili ya mchakato wa zabuni